Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Ofisi ya Makamu wa Rais



# MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI KITAIFA, BUTIAMA, MARA

1 – 4 JUNI 2017


BOY



TUKUTANE
BUTIAMA
Mazingira ni Maisha

# YALIYOMO


Tamko la Waziri ........................................................................................ 1

Kaulimbiu ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani 2017................. 2

Kwanini tunaadhimisha Kitaifa Kijijini Butiama?....................................... 4

Shughuli zitakazofanyika Butiama wakati wa Maadhimisho........................ 5

Mada zitakazotolewa na kujadiliwa ............................................................ 7

Ratiba ya Siku ya Kwanza - Tarehe 4 Juni 2017........................................... 7

Maelezo kuhusu Mada, Jopo (Panels) na wanajopo (Panelists).................... 7

Ratiba ya Siku ya Pili - Tarehe 4 Juni 2017.................................................. 12

Maelezo kuhusu Kongamano la Kitaifa kuhusu
Mazingira na Mustakabali wa Taifa 4 Juni 2017.......................................... 13

Wasifu wa Baba wa Taifa.............................................................................. 14

Namna ya kufika Butiama.............................................................................. 14



# TAMKO LA WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA) NDUGU JANUARY MAKAMBA (MB)

Kila tarehe 5 Juni, kila mwaka Watanzania tunaungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani. Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliamuliwa na Baraza la Umoja wa Mataifa la mwaka 1972, wakati wa mkutano wa kwanza wa Umoja wa Mataifa uliohusu Mazingira huko Stockholm, nchini Sweden. Aidha, Azimio la kuunda Shirika la Umoja wa Mataifa la kushughulikia Mazingira Duniani, yaani United Nations Environment Programme (UNEP) lilipitishwa pia siku hiyo. Tangu wakati huo, nchi mbalimbali duniani zimekuwa zikiadhimisha Siku ya Mazingira Duniani kila mwaka tarehe 5 Juni, kwa ujumbe maalumu unaotolewa na Umoja wa Mataifa.

Madhumuni ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ni kuhamasisha jamii duniani kote kuelewa masuala yahusuyo Mazingira na pia kuhamasisha watu wa jamii mbalimbali duniani kuwa mstari wa mbele katika kuchukua hatua za kuhifadhi na kulinda mazingira. Aidha, tunatumia siku hii kutoa fursa kwa jamii kufahamu kwamba wao wana wajibu wa kuzuia madhara na mabadiliko hasi katika Mazingira na kuhamasisha jamii kufanya mazingira yao kuwa salama na masafi ili sote tufurahie hali hiyo katika maisha yetu na vizazi vyetu.

Mwaka huu, kimataifa maadhimisho haya yanafanyika nchini Canada. Maamuzi ya kupeleka maadhimisho haya nchini Canada ni kutokana



Pamoja na kaulimbiu ya kimataifa, kaulimbiu yetu ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira mwaka huu kitaifa ni Hifadhi ya Mazingira: Muhimili kwa Tanzania ya Viwanda." Tumeamua tuwe na kaulimbiu hiyo ili kuhamasisha utunzaji wa mazingira wakati tunapokuza maendeleo ya viwanda nchini mwetu.

Kaulimbiu ya mwaka huu inatukumbusha tunavyoelekea kwenye uchumi wa viwanda tuzingatie hifadhi ya mazingira. Mara kwa mara tumeshuhudia katika uzalishaji wa viwanda mazingira asilia huharibiwa sana, hususan, kwa taka zitokanazo na uzalishaji na utupwaji wake. Kaulimbiu ya kitaifa inahimiza wazalishaji viwandani kuzingatia usimamizi endelevu wa taka zitokazo viwandani, uzalishaji wa bidhaa kwa viwango vinavyotakiwa na utumiaji endelevu wa bidhaa zinazozalishwa viwandani. Utiririshwaji ovyo wa maji machafu na utupaji ovyo wa taka za viwandani umepelekea kuwepo kwa uharibifu mkubwa wa mazingira asilia, hususan, ardhi na hewa. Kaulimbiu hii kitaifa inahamasisha wamiliki wa viwanda na wazalishaji wa bidhaa za viwandani washiriki kikamilifu katika kutunza na kuhifadhi mazingira asili kwa kuhifadhi na kutupa taka kwenye maeneo husika na kuondoa sumu kwenye maji machafu yatokanayo na uzalishaji viwandani.

na nchi hiyo kuwa na maeneo mengi yenye mazingira asili ya ardhi na maji ukilinganisha na nchi zingine. Kitaifa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yatafanyika katika kijiji cha Butiama, Mkoani Mara, siku ya Jumamosi tarehe 3 Juni na Jumapili tarehe 4 Juni.

## Kaulimbiu ya Maadhimisho 2017

Kaulimbiu inayoongoza maadhimisho haya kimataifa ni "Connecting People to Nature". Kwa Kiswahili ni: "Mahusiano Endelevu Kati ya Binadamu na Mazingira". Kaulimbiu hii inahamasisha jamii kuwa na urafiki endelevu na mazingira asilia ambapo kila mtu anapaswa kutambua, kufurahi, kujivunia na kulinda uzuri wa mazingira asilia yetu na kuhamasishana kuyatunza na kuhifadhi.



Sote tunafahamu kwamba zipo nchi hapa duniani zilizoharakisha maendeleo ya viwanda bila kuzingatia kanuni za uhifadhi wa mazingira na leo tunaona jinsi ambavyo wanahangaika kusafisha kwa gharama kubwa hewa na maji yaliyochafuliwa. Tunashuhudia katika nchi hizo kwamba kuna nyakati shule zinafungwa, ofisi zinafungwa, wananchi wanalazimishwa kutotoka nje ya nyumba zao kwa sababu hewa imechafuka kupita kiasi kutokana na moshi wa viwandani. Kwa kuwa tumeona gharama hiyo kubwa ya uchafuzi wa mazingira, ni muhimu sisi tukajifunza na kutofanya makosa waliyoyafanya wenzetu.

Kwa msingi huo, ninatoa wito kwa wamiliki, wazalishaji wa viwanda, pamoja na wananchi wote kwa ujumla kutumia fursa ya maadhimisho haya kuhakikisha maendeleo ya viwanda hayaathiri mazingira asilia ya nchi yetu ambayo ni hazina ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Katika maadhimisho ya mwaka huu, ili kuendana na kaulimbiu ya kimataifa ya kuwaweka watu karibu na mazingira ya asili, tumeamua kutoa fursa ya wananchi kutembelea katika mbuga za wanyama na hifadhi za taifa bila kulipia ada ya kiingilio ili kujionea na kufurahia mazingira asilia wanamoishi wanyama wetu. Tumefanya hivi ili kila mwananchi apate fursa ya kujifunza ili kujali na kufurahia mazingira yetu asilia na kuleta mtazamo wa kuwa na mahusiano endelevu na rasilimali zetu. Ofa hii itakuwepo kwa muda wa siku tatu kuanzia tarehe 2 hadi tarehe 4 Juni 2017.



# Kwa nini Tunaadhimisha Kitaifa Kijijini Butiama?

Kama nilivyoeleza awali, mwaka huu maadhimisho ya kitaifa yatafanyika katika kijiji cha Butiama, Mkoani Mara, ambako Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, alizaliwa, kukulia na kuzikwa. Madhumuni ya kupeleka maadhimisho haya Butiama ni kumuenzi Baba wa Taifa kwa sababu alikuwa mwanamazingira namba moja nchini mwetu lakini pia tunaenzi na kukumbuka mchango wake mkubwa katika masuala ya kuhifadhi mazingira nchini. Bila msimamo wa Mwalimu Nyerere kuhusu hifadhi ya mazingira, bila falsafa yake kuhusu uhifadhi, na bila hatua madhubuti alizochukua kulinda mazingira ya asili ya nchi yetu mapema kabisa tulipopata uhuru, nchi yetu isingekuwa inasifika kwa uzuri wake na vivutio vyake.

Kwa bahati mbaya, kila tunapomzungumzia Mwalimu Nyerere, na yote mazuri aliyolifanyia taifa letu, huwa tunasahau mchango wake mkubwa katika hifadhi ya mazingira asili ya nchi yetu. Leo hii, nchi yetu imehifadhi karibu asilimia 40 ya eneo lote la nchi, kwa sababu ya msingi wa uhifadhi aliouweka mapema kabisa katika uhai wa taifa letu.

Baba wa Taifa kila mara alisisitiza suala la umuhimu wa kutunza mazingira kwa vizazi vya sasa na vijavyo. Maneno haya aliyasema akiwa ndani na nje ya nchi. Moja ya msisitizo wake uko kwenye Ilani ya Arusha ya tarehe 21 Septemba mwaka 1961 inayohusu uhifadhi wa wanyamapori na mazingira ya asili, ambapo anasema:

> "*Uhai na uhifadhi ya wanyamapori ni suala linalotakiwa kuzingatiwa na kila mmoja wetu barani Afrika. Viumbe hawa wa porini, pamoja na mapori wanamoishi, si kwamba ni muhimu pekee kama chanzo cha kivutio cha maajabu ya asili, lakini pia ni sehemu muhimu ya maliasili yetu na ustawi wa maisha yetu ya baadaye.*
>
> *Kwa kukubali dhamana ya kuwahifadhi wanyamapori wetu tunakubali kwa dhati kwamba tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha kuwa watoto na wajukuu wetu watakuwa na fursa ya kufurahia urithi huu mkubwa na wa thamani.*
>
> *Hifadhi ya wanyamapori na maeneo ya hifadhi inahitaji kuwepo kwa ujuzi wa kitaalam, wataalam waliobobea na rasilimali fedha. Aidha, tunahitaji mataifa mengine kushirikiana na sisi katika jukumu hili muhimu - kufanikiwa au kutofanikiwa kwa uhifadhi wa maliasili hizi siyo tu kwamba utaathiri Bara la Afrika peke yake bali ulimwengu wote pia*".
>
> - Mwl. J.K. Nyerere
> 21 Sept 1961

Hivyo hatuna budi tukumbuke msisitizo wake na tumuenzi kwa kutekeleza yale aliyotamani nchi ya Tanzania na ulimwengu wote kwa ujumla kuyaona yanatendeka kwa vitendo.

# Shughuli Zitakazofanyika Butiama Wakati wa Maadhimisho

**1** **Kupanda miti na kutangaza hatua za kuuhifadhi na kuulinda msitu ambao Baba wa Taifa aliuhifadhi.**

Tutakapokuwa Butiama tutashuhudia kazi ya mikono ya Baba wa Taifa katika kuhifadhi mazingira. Tutapata ushuhuda wa moja kwa moja kutoka kwa wanafamilia na watu wengine waliofanya kazi naye kuhusu jitihada zake na moyo wake wa dhati wa kutunza na kuhifadhi mazingira. Tutatembelea msitu wake alioupanda na kuutunza na ambao sasa unapata changamoto za uharibifu. Tutashiriki katika kupanda miti katika msitu ule na kuchukua hatua nyingine za kuulinda na kuuhifadhi, kama sehemu ya kukumbuka na kuenzi kazi za Baba wa Taifa.

**2** **Kuendesha mijadala (katika mfumo wa majopo – panels) kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu maisha ya Watanzania, shughuli wanazofanya na hifadhi ya mazingira.**

Siku ya Jumamosi, tarehe 3 Juni 2017, kutaendeshwa mijadala mbalimbali inayohusu umuhimu wa hifadhi ya mazingira kwa maendeleo ya sekta muhimu za uchumi wa nchi. Kutakuwa na mada nne, zitakazoendeshwa kwa mfumo wa majopo (panels) la wataalam na wadau kutoka sekta binafsi, wataalam/watafiti, kutoka Serikalini, na wanaharakati wa mazingira. Madhumuni ya mijadala hii ni kuonyesha kwamba bila hifadhi ya mazingira, maendeleo katika sekta muhimu za uchumi na huduma, ikiwemo kilimo, uvuvi, utalii, mifugo, nishati na maji, hayataweza kupatikana, au hata yakipatikana, basi hayatadumu. Mijadala hii ina lengo la kutafuta majawabu kuhusu mbinu za kuhifadhi mazingira na kuweka hifadhi ya mazingira katikati ya mipango na mikakati ya maendeleo ya sekta zote za uchumi na huduma za jamii.

Mada zitakazotolewa na wanajopo (panellists) zimeanishwa kwenye kijitabu hiki.



3 **Kuendesha Kongamano la viongozi kuhusu mchango wa Mwalimu Nyerere kwenye hifadhi ya mazingira nchini na umuhimu wa mazingira kwa mustakabali wa nchi yetu na masuala ya msingi ambayo Baba wa Taifa aliyasisitiza.**

Siku ya Jumapili, tarehe 4 Juni 2017, kutaendeshwa Kongamano la Kitaifa la Mazingira, ambalo litamshirikisha Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na viongozi wengine na wanafamilia wa Baba wa Taifa, kuhusu mchango wa Mwalimu Nyerere katika hifadhi ya mazingira nchini na nafasi ya hifadhi ya mazingira kwa mustakabali wa taifa letu. Madhumuni ya Kongamano hili ni kutumia mfano na maisha ya Mwalimu Nyerere kama chachu ya kuhimiza na kuhamasisha hifadhi ya mazingira nchini. Vilevile, tunatarajia kupata mwelekeo wa taifa letu kutokana na hali ya uharibifu wa mazingira ilivyo sasa na mbinu na msukumo katika ngazi ya uongozi wa kisiasa kukabiliana na hali hiyo.

4 **Maonesho ya shughuli za mazingira.**

Vilevile, kutakuwa na maonesho ya shughuli za hifadhi ya mazingira katika mabanda ya taasisi na vikundi mbalimbali.

"Napenda kuwakaribisha Watanzania wote katika maadhimisho haya. Kijiji cha Butiama kina nafasi muhimu katika historia ya nchi yetu. Maadhimisho haya yanatoa fursa kwetu sote kufika kijijini pale, ambako pia kuna Jengo la Makumbusho ya Taifa (National Museum) lililobeba Makumbusho ya Mwalimu Nyerere.

Vilevile, katika kipindi hiki cha kuelekea katika maadhimisho haya, nawasihi Watanzania wote kwamba tusimuonee aibu mtu yeyote endapo tutamwona anafanya shughuli au vitendo vinavyoharibu mazingira yetu na hana nia njema ya kuacha urithi kwa vizazi vijavyo. Kwani mtu huyu atakuwa hafanyi vitendo vinavyoashiria mahusiano endelevu kati yake na mazingira. Hivyo, tusisite kutoa taarifa za watu kama hao kwenye mamlaka husika ili hatua stahiki dhidi yao zichukuliwe mara moja.

Tunapoadhimisha Wiki ya Mazingira tuanze na tuendelee kumuenzi Baba wa Taifa kwa kufanya kila siku kuwa ni siku ya mazingira kwa kufanya shughuli za usafi kwenye maeneo ya viwanda, sokoni, barabarani na maeneo tunayoishi, kupanda miti kila wakati maeneo ambayo mvua inanyesha, kuhifadhi sehemu husika taka tunazozizalisha majumbani na katika shughuli za kiuchumi na tuwe na uzalishaji endelevu viwandani. Pia tujielimishe sana ili matendo ya maisha yetu yalenge kuongeza utunzaji wa mazingira yetu.

Mwisho, napenda kuvipongeza vyombo vya habari kwa kazi nzuri ya uhamasishaji na ukuzaji weledi kwa wananchi juu ya masuala ya mazingira. Naomba vyombo vya habari viendeleze juhudi hizi za kuelimisha umma kwamba kila mtu awe na mahusiano endelevu na mazingira na kupambana dhidi ya uharifu wa mazingira yetu. Tunatambua kwamba vyombo vya habari vina nafasi na uwezo mkubwa wa kuifikia jamii na naamini mnaweza kusaidia sana katika suala hili."



# MADA ZITAKAZOTOLEWA NA KUJADILIWA TAREHE 3 JUNI 2017 BUTIAMA

Kama ilivyoelezwa awali, kwa siku ya kwanza, tarehe 3 Juni 2017, kutakuwepo na mijadala mbalimbali inayohusu umuhimu wa hifadhi ya mazingira kwa maendeleo ya sekta muhimu za uchumi wa nchi. Kutakuwa na mada nne, zitakazoendeshwa kwa mfumo wa majopo (panels) ya wataalam na wadau kutoka sekta binafsi, wataalam/watafiti,kutoka Serikalini na wanaharakati wa mazingira. Wananchi pia watashiriki kujadili, kuuliza maswali, na kutoa maoni na ushauri. Majadiliano ya mada hizo yatakuza uelewa wa wananchi katika maeneo yatakayojadiliwa na kuhamasisha wananchi kuchukua hatua stahiki.

**Ratiba ya Mada Siku ya Kwanza, 3 Juni 2017**

| Muda | Mada |
|---|---|
| Saa 2:30 asubuhi – 3:00 asubuhi | Maelezo ya awali ya ufunguzi |
| Saa 3:00 asubuhi – 4:30 asubuhi | Tanzania Bila Mkaa na Kuni Inawezekana? |
| Saa 4:30 asubuhi – 5:00 asubuhi | Mapumziko mafupi. |
| Saa 5:00 asubuhi – 6:30 mchana | Gharama ya Uharibifu wa Mazingira kwa Uchumi wa Nchi: Athari kwa Sekta za Kilimo, Ufugaji, Uvuvi na Utalii. |
| Saa 6:30 mchana – 8:00 mchana | Mapumziko ya chakula cha mchana |
| Saa 8:00 mchana – 9:30 alasiri | Nafasi ya Imani ya Dini Katika Hifadhi ya Mazingira. |
| Saa 9:30 alasiri – 10:00 alasiri | Mapumziko mafupi. |
| Saa 10:00 alasiri – 11:30 jioni | Mafunzo na Urithi wa Mwalimu Nyerere Katika Hifadhi ya Mazingira ya Butiama. |

## Maelezo Kuhusu Mada, Jopo (Panels) na Wanajopo (Panelists)

**MADA YA KWANZA**

## Tanzania Bila Mkaa na Kuni Inawezekana?

**Muda -** SAA **3:00 – 4:30** ASUBUHI

**Maelezo Mafupi ya Mada:**

Hali ya uteketezaji wa misitu ni ya kutisha nchini. Kwa sasa, takriban kila siku tunapoteza ekari 2,500 za misitu na asilimia 61 ya eneo la nchi yetu linatishiwa kuwa jangwa. Kutokana na kuteketea kwa misitu kwa kasi hii kubwa, vyanzo vya maji, ambavyo vingi vipo misituni, vinaathirika na tunashuhudia baadhi ya mito ikikauka. Kutokana na hali hii, uhakika wa upatikanaji wa huduma ya maji kwa Watanzania unapungua, hata pale tulipojenga miundombinu ya usambazaji wa maji hayo. Moja ya sababu kubwa za uteketezaji wa misitu yetu ni matumizi makubwa ya mkaa kwa ajili ya nishati ya kupikia. Biashara ya mkaa ni kubwa na inaendelea kushamiri. Asilimia zaidi ya 90 ya kaya zote nchini zinatumia aidha nishati ya kuni au mkaa. Kasi ya usambazaji wa umeme vijijini imeongezeka kwa kasi lakini bado umeme haujawa na hauwezi kuwa suluhisho la nishati ya kupikia hasa kutokana na bei. Gesi asilia imegundulika nchini na imeanza kutumika


kuzalisha umeme tangu mwaka 2004 lakini bado pia haijawa suluhisho la nishati ya kupikia. Biashara ya gesi ya kupikia kwenye mitungi (LPG) nayo inakuwa na kushamiri kwa kasi kubwa lakini nayo pia haijawa suluhisho kutokana na bei ya mitungi na mtandao wa vituo vya kusambazia gesi hiyo kuwa bado mdogo, lakini pia kutokana na wasiwasi kuhusu usalama wa gesi hiyo. Aidha, utamaduni na imani kwamba baadhi ya vyakula haviwezi kupikwa kwa gesi imekuwa changamoto. Jiji la Dar es Salaam, licha ya kuwa lina umeme kila mtaa, na vituo vingi vya kujazia gesi ya kupikia, ndilo linalotumia asilimia 60 ya mkaa wote unaozalishwa nchini. Mahitaji ya nishati ya mkaa ni makubwa katika maeneo ya mijini na yataendelea kuongezeka. Hali hii inasababisha changamoto kubwa katika suala zima la hifadhi ya misitu kwa ujumla. Hivyo, bila kuwepo na suluhisho la uhakika kuhusu suala hili bado misitu itaendelea kuteketezwa. Jopo hili litategemewa kufunua macho Watanzania kuhusu mwelekeo wa suluhisho la nishati ya kupikia kwa Watanzania wa hali ya chini. Baadhi ya vipengele vitakavyojadiliwa katika jopo hili ni pamoja na hali ilivyo sasa ya matumizi ya mkaa utokanao na misitu nchini; uzalishaji hadi matumizi ya mkaa nchini (charcoal value chain); athari zitokanazo na matumizi ya mkaa; changamoto za kuondokana na matumizi ya mkaa; mbadala wa mkaa nchini ni nini na nini kifanyike mbadala huo utoe ushindani kwa mkaa? Nini kifanyike kupunguza matumizi ya mkaa?

Mchokoza Mada: **Prof. Romanus Ishengoma**, Profesa wa Misitu, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA)

Wanajopo (Panellists):

1. **Eng. Estomih Sawe** - Mkurugenzi Mtendaji, TaTEDO, Center for Sustainable Modern Energy Initiative in Tanzania;
2. **Profesa Dos Santos Silayo** – Mkurugenzi Mkuu, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS);
3. **Ndugu Charles Meshack** – Mkurugenzi Mkuu, Shirika la Kuhifadhi Misitu Asili Tanzania (TFCG); na
4. **Ndugu Ally Awadh** – Mmiliki na Afisa Mtendaji Mkuu wa Lake Group.

Mwendesha Mada (Moderator): **Maria Sarungi**



# Gharama ya Uharibifu wa Mazingira kwa Uchumi wa Nchi: Athari kwa Sekta za Kilimo, Ufugaji Uvuvi na Utalii.

**Muda** - SAA **5:00** ASUBUHI – **6:30** MCHANA

**Maelezo ya Mada:**

Kumekuwa na mazoea ya kudhani kwamba huduma zipatikanazo na utumiaji wa maliasili haina gharama yoyote (free service) au kama gharama hiyo imewahi kufikiriwa basi ilipewa thamani ndogo kuliko ilivyostahili (underpricing). Kwa mfano, miti asili imekatwa bila kulipiwa, maji kutoka kwenye mito, mabwawa na maziwa yametumika bila malipo yoyote, samaki wamevuliwa bila malipo yoyote. Ukataji miti, utumiaji wa maji na uvuvi ni shughuli za kiuchumi ambazo zinamletea mwanadamu faida na hivyo maendeleo ya kiuchumi. Ni muhimu sasa tuanze kutambua thamani ya mazingira yetu. Tafiti mbalimbali zimeonesha kuwa ukuaji wa uchumi wa nchi una mahusiano ya karibu na hali ya mazingira ya nchi husika. Maliasili kutoka kwenye mazingira zinavyotumika kwa wingi uchumi wa nchi hukua kwa haraka na wakati huo upatikanaji wa maliasili hizo hupungua. Utafika wakati ambapo maliasili hizo hazitoshi tena kuendeleza ukuaji wa uchumi kwa sababu mazingira yatakuwa yameharibika. Ikifikia hapo kutakuwa na gharama kubwa ya kuharibika kwa mazingira (environmental damage cost) na ya kurekebisha uharibifu huo (maintenance cost).

Kwa kuwa mazingira ni mifumo ya ikolojia inayotegemeana, uharibifu wa ikolojia mojawapo huleta athari kwa mfumo mzima wa ikolojia. Kwa mfano ukataji wa miti husababisha upungufu wa mvua ambayo itasababisha kupungua kwa maji kwenye mito, mabwawa na maziwa. Upungufu wa maji huathiri shughuli za kiuchumi kwenye kilimo, nishati, ufugaji na uvuvi. Aidha, upungufu na uchafuzi wa maji huleta athari za kiafya kama vile magonjwa ya kuambukiza. Gharama ya kurekebisha mazingira yaliyoharibika ni kubwa kuliko gharama ya kuzuia uharibifu wa mazingira usitokee. Hivyo kuwekeza katika usimamizi wa mazingira ni jambo lisiloepukika kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi.

Kitaifa suala la gharama ya uharibifu wa mazingira kwa uchumi wa nchi halijapata mjadala wa kina. Kwa kuzingatia kuwa uchumi wa nchi yetu na maendeleo ya viwanda kwa ujumla vinategemea utumiaji wa maliasili, kuna haja ya kulijadili jambo hili kwa upana kwa ajili ya kupata muafaka unaostahili.

Mchokoza Mada: **Profesa Razack Lokina** – Mhadhiri Mwandamizi, Uchumi na Mazingira, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM)

Wanajopo (Panelists)

1. **Inj. Seth Luswema** – Wizara ya Maji na Umwagiliaji.
2. **Dkt. James Wakibara** – Hifadhi ya Taifa ya Saadani (SANAPA).
3. **Ndugu Conrad Ndomba** – Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.
4. **Profesa Yunus Mgaya** – Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Dhamana wa Mazingira.

Mwendesha Mada (Moderator): **Ndugu Ali Mufuruki**, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Mazingira;





MADA YA TATU

# Nafasi ya Imani ya Dini Katika Hifadhi ya Mazingira.

**Muda - SAA 8:00 MCHANA – 9:30 MCHANA**

**Maelezo ya Mada:**

Serikali ya Tanzania haina dini. Kwa msingi huo, sera, sheria na mipango ya Serikali haitengenezwi kwa misingi au miongozo ya dini yoyote. Hata hivyo, Watanzania walio wengi ni waumini wa dini mbalimbali na wanafuata miongozo ya dini zao katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Ni dhahiri pia kwamba waumini wanawasikiliza na kufuata maneno ya viongozi wao wa kiimani kwenye masuala mengi ya kijamii. Mara kadhaa, viongozi wa Serikali wamekuwa wakiwaomba viongozi wa dini watoe ushirikiano katika kuhimiza masuala muhimu ya kitaifa. Vilevile, tumeshuhudia mara kadhaa, viongozi wa dini wakitoa wito na miongozo kwa waumini wao kuhusu umuhimu wa hifadhi ya mazingira, mfano wa hivi karibuni ukiwa ni ujumbe wa Kwaresma wa mwaka 2017 kutoka kwa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania. Baadhi yao wameeleza kwamba kwamba kuharibu mazingira ni kuharibu kazi ya Mungu ya uumbaji. Katika mada hii, viongozi wa dini wataongoza mjadala kuhusu suala hili na kuelezea kuhusu nafasi ya imani ya dini na maelekezo ya muumba wetu kuhusu hifadhi ya mazingira.

Mchokoza Mada: **Mhe. Profesa Palamagamba Kabudi** (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria;

Wanajopo (Panelists)

1. **Sheikh Khamis Saidi Mataka** - Mwenyekiti wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA).
2. **Mhashamu Askofu Dkt George Okoth** – Askofu wa Kanisa la Anglikana, Dayosisi ya Mara.
3. **Padri Raymond Saba** - Katibu Mkuu, Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania.
4. **Subash Patel** – Mdhamini Shree Hindu Mandal Tanzania.

Mwendesha Majadiliano (Moderator): **Dkt. Richard Sembaiga**, Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Soshiolojia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.





MADA YA NNE

# Mafunzo na Urithi wa Mwalimu Nyerere Katika Hifadhi ya Mazingira ya Mwitongo na Butiama.

**Muda - SAA 10:00 ALASIRI – 11:30 JIONI**

**Maelezo ya Mada:**

Kwa elimu, Mwalimu Nyerere alikuwa mwanafunzi wa biolojia na hasa biolojia ya mimea (botany) na alifundisha somo hilo. Kwahiyo, kwa asili Mwalimu aliijua na aliipenda mimea na kutambua thamani yake na haja ya utunzaji wa mazingira. Ushuhuda wa Mwalimu Nyerere kuthamini hifadhi ya mazingira, unaoneka kwa hatua kubwa, madhubuti na za kijasiri alizochukua akiwa kiongozi wa nchi, hatua zilizopelekea takriban asilimia 40 ya nchi yetu kuhifadhiwa. Vilevile, ushuhuda huo unaonekana kwenye makazi yake Mwitongo na kijijini kwake Butiama kwa ujumla, ambapo alihifadhi mazingira ya asili ikiwemo msitu wa asili.

Mwalimu aliyoyaamini aliyatekeleza kwa vitendo. Mwalimu alifundisha wananchi wa kijiji cha Butiama kuwa wahifadhi na watunza mazingira. Mwaka 1985 alipostaafu aliufufua msitu wa matambiko ya Wazanaki unaoitwa msitu wa Muhunda wenye ekari 15, kwani Wazanaki walikuwa wamevunja miiko ya msitu huo kwa kuuvamia na kuuharibu baada ya baba yake Mwalimu Nyerere kufariki. Aidha, mwaka 1985 aliuzungushia uzio msitu huo wa matambiko kwa kupanda miti ili kuulinda msitu huo. Kwa kufanya hivyo akawa ameanzisha msitu wake unaoitwa msitu wa Mwalimu Nyerere ambao una hekari 52.

Mwaka huo huo alianzisha vitalu vya miti kwa kuwahusisha wataalamu wa Hifadhi Ardhi Dodoma (HADO) na Arusha kwa lengo la kuwapa mafunzo kwa vitendo Wazanaki kwa kugawa miche shuleni.

Kiasilia Wazanaki hawakuwa na utamaduni wa kupanda miti ila Mwalimu aliwaonesha kwa vitendo wapende kupanda miti na kuitunza. Katika juhudi hizo aliwashawishi kijiji cha Butiama kupanda miti kwenye miinuko na vilima. Lengo lilikuwa kupunguza upepo mkali maeneo hayo. Faida na juhudi za Mwalimu zinaonekana leo.

Kuna msemo kwamba "mifano ya watu wema, hutengeneza watu wema". Mwalimu Nyerere, kama mwanakijiji, aliweza kuonyesha njia jinsi gani mwananchi wa kawaida, pale alipo, anaweza kutunza na kuhifadhi mazingira yake. Kwa kuwa wengi wetu tunatamani kumuenzi Mwalimu Nyerere, tamaa hiyo itatimia kwa kuishi kwa mfano wake. Katika mada hii, tutapata ushuhuda kutoka kwa wanafamilia na wanakijiji wa Butiama jinsi Mwalimu Nyerere alivyofanya jitihada binafsi za kuhifadhi na kutunza mazingira.

Mchokoza Mada: **Emmanuel Kiondo**, Mkurugenzi wa Makumbusho ya Mwalimu Nyerere, Butiama.

Wanajopo (Panelists):

1. **Chifu Japhet Wanzagi** – Mwanafamilia
2. **Profesa Raphael Mwalyosi** – Alifanya kazi za uhifadhi na Baba wa Taifa
3. **Ndugu Madaraka Nyerere** – Mwanafamilia

Mwendesha Majadiliano (Moderator): **Mwalimu Magoma Lugora**, Mwalimu Mkuu, Shule ya Sekondari Buturugi, Mara

# RATIBA YA SIKU YA PILI - TAREHE 4 JUNI 2017

(Mwendesha Shughuli: **Maria Sarungi**)

| Muda | Shughuli | Mhusika |
|---|---|---|
| 12:30 – 2:00 asuhuhi | Misa Kanisani Butiama | Waumini |
| 2:30 – 4:00 asubuhi | Kupanda Miti – Msitu wa Mwalimu Nyerere | Wote |
| 4:30 asubuhi – 6:30 mchana | Mkutano na Wananchi – Uwanja wa Mwenge Butiama | Mkuu wa Mkoa<br><br>Makamu wa Rais |
| 6:30 mchana – 8:30 mchana | Mapumziko | Wote |
| 8:30 mchana – 11:30 jioni | Kongamano Kuhusu Mchango wa Mwalimu Nyerere Kwenye Hifadhi ya Mazingira na Umuhimu wa Hifadhi ya Mazingira kwa Mustakabali wa Taifa | Wote |



# Maelezo Kuhusu Kongamano la Kitaifa Kuhusu Mazingira na Mustakabali wa Taifa 4 Juni 2017

Tanzania ni nchi inayosifika kote duniani kwa mandhari nzuri, mazingira ya asili, na utajiri wa maliasili. Kwa miaka zaidi ya 50 sasa, Watanzania wametumia mazingira ya asili na utajiri wa maliasili katika kuendesha shughuli za kujitafutia maisha. Vilevile, kwa upande wa Serikali, mipango ya maendeleo ya sekta muhimu za uzalishaji, ikiwemo kilimo, ufugaji, uvuvi na utalii, imetegemea kuwepo kwa rasilimali zitokanazo na mazingira ya asili, ikiwemo ardhi, mito, maziwa, bahari, wanyamapori, na misitu. Kwa msingi huo, maendeleo ya Watanzania yamefungamana na mazingira. Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, alitambua hili na mara kadhaa alilizungumzia kufungamana huku, akiwa madarakani na hata baada ya kustaafu. Hata kabla ya Tanzania kupata uhuru wake, mnamo mwezi Septemba 1961, Mwalimu Nyerere alitoa kauli nzito kuhusu haja na umuhimu wa kuhifadhi mazingira, kauli ambayo inaitwa Ilani ya Arusha (Arusha Manifesto) ambayo iliweka msingi wa uhifadhi nchini. Ushuhuda wa Mwalimu Nyerere kuthamini hifadhi ya mazingira, unaoneka kwa hatua kubwa, madhubuti na za kijasiri alizochukua akiwa kiongozi wa nchi, hatua zilizopelekea asilimia 40 ya nchi yetu kuhifadhiwa. Vilevile, ushuhuda huo unaonekana kwenye makazi yake Mwitongo na kijijini kwake Butiama kwa ujumla, ambapo alihifadhi mazingira ya asili ikiwemo msitu wa asili pamoja na bwawa la maji.

Kila mwaka, huwa tunajikumbusha kuhusu kumuenzi Mwalimu Nyerere na yale aliyoyasimamia. Hata hivyo, kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira unaoendelea nchini, ni dhahiri kwamba tumepotoka na tumejisahau kusimamia jambo ambalo Mwalimu alilithamini sana. Moja ya madhumuni ya kongamano hili ni kukumbushana kwamba hatuwezi kumuenzi Mwalimu kwa kuchagua ni mambo gani tunayaenzi na yapi tunayapuuza. Kongamano litajadili kuhusu mchango wa Mwalimu Nyerere katika kuhifadhi mazingira nchini. Kongamano pia litajadili kuhusu mustakabali wa nchi yetu na hatari tunayokabiliana nayo kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira nchini. Kongamano linatarajiwa kutoa msukumo mpya kwa uongozi wa kisiasa nchini kuyapa masuala ya masuala ya mazingira kipaumbele kama nyenzo muhimu ya maendeleo ya nchi. Kongamano hili litahudhuriwa na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na viongozi mbalimbali wa kisiasa na kijamii na wananchi kwa ujumla, ambao watashiriki katika mjadala. Aidha, Kongamano litafungwa na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na litatangazwa moja kwa moja na vituo vya televisheni na redio.

**Muda wa Kongamano: Saa 8:30 mchana – 11:30 jioni**

Wazungumzaji Wakuu:

1. **Mhe. Profesa Palamagamba Kabudi** (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria;
2. **Ndugu Ali Mufuruki**, Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Taifa wa Mazingira;
3. **Dkt. Felician Kilahama**, Mkurugenzi Mstaafu wa Idara ya Misitu na Nyuki;

**Mwendesha Mada (Moderator): Maria Sarungi**

**Kufunga Kongamano/Maadhimisho:**

**Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

A.

# MAELEZO YA ZIADA

**Historia ya Kijiji cha Butiama**

Maana ya neno Butiama imetokana na Wajerumani kuita eneo kulingana na wakazi wa eneo husika. Hivyo kwa kuwa wakazi wa eneo hilo walikuwa wanaitwa Watiama, Wajerumani wakaita eneo hili Butiama. Kijiji kipo katika Wilaya mpya ya Butiama, Mkoa wa Mara.


Kabla ya ukoloni, Butiama ilitawaliwa kwa mtindo wa Uchifu. Machifu walioongoza Butiama miaka ya karibuni ni wafuatao: Chifu Buhoro; Chifu Nyerere Burito; Chifu Wanzagi Nyerere na Chifu Japhet Wanzagi ambaye yupo madarakani sasa. Wakazi wa Butiama ni Wazanaki ambao wamegawanyika katika koo mbalimbali kama vile: Bakibagara, Bangoye, Bibugu, Biraburu.

Kijiji cha Butiama kimepakana na vijiji jirani kadhaa. Kwa upande wa mashariki kimepakana na Kijiji cha Bumangi; kaskazini kimepakana na Kijiji cha Busegwe; kusini kimepakana na Kijiji cha Bisarye na magharibi kimepakana na Mwanza Buriga na Kiabakari. Kijiji kina eneo la hekta 9,080 na kilipata hati miliki ya miaka 99 yenye namba 3559 iliyotolewa mwaka 1988. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 kijiji kina jumla ya watu 10,306.

Butiama imejulikana kimataifa kwa sababu ni mahali ambako alizaliwa Rais wa kwanza wa Tanganyika halafu wa Tanzania Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Katika kijiji hicho, makazi ya Mwalimu Nyerere yapo kwenye kitongoji cha Mwitongo. Katika kipindi chote cha uongozi wake, Mwalimu Nyerere, kila wakati alipohitaji, alikuwa akienda mapumzikoni Butiama ambako alijishughulisha na shughuli za kilimo. Aliendelea kuwa na nyumba kijijini hapo, ambako alirudi baada ya kustaafu kama Rais na baadaye pia kama Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Mapinduzi (CCM). Baada ya kufariki kwake tarehe 14, Oktoba 1999, alizikwa huko. Sasa makazi yake yamekuwa Nyumba ya Makumbusho. Viongozi wengi wa kisiasa na kijamii, pamoja na watu kutoka ndani na nje ya nchi, hutembelea Butiama kuona pahala Mwalimu Nyerere alipozaliwa na kuzikwa.

## Wasifu wa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere

Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa Rais wa kwanza wa Tanganyika kuanzia mwaka 1961 na hatimaye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1964 hadi alipong'atuka mwaka 1985. Mwalimu Nyerere alizaliwa tarehe 13 Aprili 1922 katika kijiji cha Mwitongo, Butiama mkoani Mara akiwa ni mmoja wa watoto 26 wa Chifu wa kabila la Wazanaki, Mzee Nyerere Burito. Mwalimu Nyerere alihudhuria Shule ya Msingi Mwisenge, Musoma na baadaye kwenda Shule ya Sekondari Tabora, kisha kupata nafasi ya kusoma katika Chuo Kikuu cha Makerere nchini Uganda. Baada ya kurudi nchini, alifundisha somo ya biolojia katika Shule ya Sekondari ya Mtakatifu Maria Tabora kabla ya kwenda kuchukua shahada ya uzamili huko Scotland. Baada ya kurejea aliendelea na harakati za siasa na kushiriki kuasisi chama cha TANU mwaka 1954, kilichopigania na kufanikisha kuongoza mapambano ya kupata uhuru wa Tanganyika mwaka 1961. Baada ya kupata uhuru, Mwalimu alikuwa Waziri Mkuu wa kwanza wa Tanganyika na baadaye, baada ya Tanganyika kuwa Jamhuri, akawa Rais wa kwanza wa Tanganyika, kisha Rais wa kwanza wa Tanzania baada ya Muungano katika ya Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964.




Katika kipindi chote cha uongozi wake, Mwalimu Nyerere aliazimia kujenga jamii iliyo sawa, ya haki, na yenye maendeleo yanayosukumwa na watu na yanayowagusa watu walio wengi. Vilevile, katika kipindi cha uongozi wake, na hata baada ya hapo, Mwalimu alihubiri umoja na amani. Pia katika kipindi cha uongozi wake, Tanzania iliongoza jitihada za kupigania uhuru na ukombozi wa nchi zilizokuwa zinatawaliwa.

Mwalimu Nyerere alikuwa mwanamazingira wa kweli. Mwalimu alisomea na kufundisha biolojia, hasa sayansi ya mimea (botany). Aliipenda na kuijua sana mimea na umuhimu wa uhifadhi wake kama sehemu ya mazingira yetu. Katika jitihada za kuhifadhi mazingira alichukua hatua madhubuti kabisa za kuhifadhi sehemu kubwa ya nchi yetu. Katika nyanja za kimataifa, alitetea msimamo wa kufungamanisha maendeleo na hifadhi ya mazingira. Pia alitoa matamko mbalimbali ambayo ni pamoja na Ilani ya Arusha iliyohusu uhifadhi wa wanyapori ya mwaka 1961. "Uhai wa wanyamapori ni jambo linalotuhusu sisi sote katika Afrika, viumbe hai wa porin, pamoja na mapori waishimo, sio muhimu tu kwa ajili ya kuajabiwa na kuvutia lakini pia ni sehemu ya maliasili yetu na mustakabali wa maisha yetu ya badaaye". Aidha, katika Ilani ya Arusha alisema ..."tufanye kila tuwezalo kuhakikisha kuwa watoto na wajukuu wetu watakuwa na fursa ya kufurahia urithi huu mkubwa".

Vilevile, Mwalimu Nyerere alitoa mchango wake akisisitiza umuhimu wa hifadhi ya mazingira ndani na nje na hii inadhihirishwa kwa vitendo ambapo Mwalimu mwenyewe aliweza kutunza vizuri mazingira ya kijijini Butiama ikiwa ni pamoja na kuhifadhi msitu wake wa ekari hamsini na mbili (52) za msitu wa asili.



Makumbusho ya Taifa inayosimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Makumbusho ya baba wa Taifa ni Taasisi yenye dhamana ya kutafiti, kuhifadhi na kuelimisha umma kuhusu urithi wa baba wa Taifa unaohusu historia ya maisha yake na uongozi wake kwa kizazi kilichopo na kizazi kijacho.

Wazo la ujenzi wa Makumbusho hii lilianza mwaka 1985, baada ya Baba wa Taifa kustaafu kazi ya Urais. Hata hivyo, ujenzi rasmi ulianza mwaka 1987 chini ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Jumba la Makumbusho lilifunguliwa rasmi tarehe 2 Julai 1999 na aliyekuwa Waziri Mkuu wakati huo Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye. Mwalimu Nyerere alishiriki sherehe za ufunguzi huo. Hata hivyo baada ufunguzi wa makumbusho hii, miezi mitatu baadaye, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alifariki dunia tarehe 14 Octoba 1999 katika Hospitali ya Mtakatifu Thomas nchini Uingereza.

Makumbusho ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere yanahifadhi mikusanyo (collections) kuhusu historia ya Baba wa Taifa na mchango wake alioutoa kimataifa, na kitaifa hususan katika nyanja mbalimbali za maendeleo ya Taifa na harakati za ukombozi wa bara la Afrika.

Makumbusho haya yanatoa taswira halisi ya wananchi wa Tanzania, tofauti zao za kitamaduni na harakati zao za kimaendeleo kabla na baada ya uhuru mwaka 1961 chini ya uongozi wa Baba wa Taifa.

Kwa ujumla makumbusho haya yana jukumu kubwa la kukusanya, kuhifandhi, kutafiti, kuelimisha na kuandaa maonesho yanayohusu historia ya maisha ya Baba wa Taifa na mchango wake kitaifa na kimataifa.



Miongoni mwa mikusanyo au vitu vilivyohifadhiwa kwenye maonesho ya makumbusho haya ni pamoja na:

- Zawadi alizopewa Baba wa Taifa na Watanzania katika harakati za kudai Uhuru na baada ya uhuru;
- Zawadi alizopewa Baba wa Taifa na Watanzania mwaka 1985 alipostaafu madaraka ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- Zawadi alizopewa Baba wa Taifa na Watanzania baada ya vita ya Kagera kama alama ya ujasiri, ushujaa na uzalendo;
- Zawadi alizopewa Baba wa Taifa na watu na serikali za mataifa mbalimbali duniani ambazo Baba wa Taifa alitembelea;
- Baadhi ya vitu binafsi vya baba wa Taifa ambavyo alivitumia katika maisha yake, kama vile nguo zake za aina mbalimbali alizozipenda kama vile suti na viatu. Vilevile makumbusho imehifadhi vifaaa alivyofanyia navyo kazi shambani kwake na picha mbalimbali alizopigwa katika matukio mbalimbali. Aidha zipo zawadi za kitaaluma alizopewa baba wa Taifa na vyuo vikuu mbalimbali duniani ( Shahada za heshima za udaktari wa Falsafa ).

Kwa ujumla Makumbusho ya Baba wa Taifa ni mahali pa kipekee ambapo watu wa rika zote wa ndani na nje ya nchi hupata fursa ya kujifunza, kufurahia na kutafakari juu ya historia ya maisha ya Baba wa Taifa katika uongozi na maisha yake ya kawaida kama Mtanzania aliyejitoa mhanga katika kuleta uhuru wa Tanzania.

Taarifa zinazopatikana katika makumbusho haya ni urithi wa kipekee aliotuachia Baba wa Taifa na ambao umehifadhiwa kwa faida ya vizazi vilivyopo na vijavyo.




*Picha hii inaonesha kaburi ulimohifadhiwa mwili wa Baba wa Taifa kitongoji cha Mwitongo-Butiama na maeneo ya nyumba yake.*

## Namna ya Kufika Butiama

Kijiji cha Butiama kipo umbali wa kilomita 48 kutoka Mji wa Musoma, ambapo kwa gari ya kawaida ni usafiri wa takriban nusu saa. Vilevile, Butiama ni takriban kilomita 180 toka jiji la Mwanza na kilomita 11 toka kijiji cha Kiabakari yaliyopo makutano ya Barabara ya Musoma-Arusha.

## Usafiri wa Anga

Kutoka Dar es Salaam kuna usafiri wa kila siku wa ndege hadi Mwanza. Siku ya Ijumaa tarehe 2 Juni, kutakuwa na basi dogo maalum kutoka airport ya Mwanza hadi Musoma kwa ajili ya washiriki wa Maadhimisho. Basi hilo litaondoka Mwanza saa kumi alasiri.

Lakini pia kutoka Dar es Salam kuna Ndege ya Precision Air ambayo huenda hadi uwanja wa Musoma kwa siku za Jumanne, Alhamisi, Jumamosi na Jumapili.

**Kwa ajili ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL), litapunguza nauli ya ndege kutoka Dar es Salaam - Mwanza - Dar es Salaam kwa siku ya Ijumaa, tarehe 2 Juni na siku ya Jumatatu, tarehe 5 Juni. Na pia kutakuwa na basi maalum kutoka Mwanza Airport hadi Musoma.**

## Usafiri wa Barabara

Kutoka Dar es Salaam kuna mabasi hadi Mwanza kila siku na pia kutoka Mwanza kuna mabasi hadi Musoma kila baada ya masaa sita. Aidha kutoka Musoma kuna mabasi hadi Butiama (Mwitongo) angalau mara tatu kwa siku.

Kutoka Arusha kuna mabasi yanayopita njia ya Karatu na mbuga ya Serengeti hadi Musoma kila siku.

Njia nyingine kwa usafiri binafsi ni kutoka Mwanza-Bunda-Kiabakari-hadi Butiama

Njia nyingine kwa usafiri binafsi ni kutoka Shinyanga-Busega-Bunda-Kiabakari hadi Butiama.

# Malazi Butiama

ORODHA YA BAADHI YA NYUMBA ZA KULALA WAGENI- MUSOMA, BUNDA NA BUTIAMA

**1.** Orodha ya nyumba za kulala wageni Manispaa ya Musoma (Umbali kutoka Musoma hadi Butiama ni Kilometa 48 au usafiri wa nusu saa)

**A -** Daraja la Kwanza

| NA | JINA LA HOTELI | SEHEMU ILIPO | MAWASILIANO | IDADI YA VYUMBA | GHARAMA YA CHUMBA |
|---|---|---|---|---|---|
| | Mara Peninsula Hotel | Makoko RD, Mwisenge | 0754505082 | 13 | 45,000 - 150,000 |
| | Mara Acacia Motel | Makoko RD, Mwisenge | 0767405889 | 10 | 50,000 – 150,000 |
| | Mara Paradise Hotel | Nyarusurya, Bweri | 0758469415 | 9 | 35,000 – 60, 000 |
| | Ngerengere Hotel | Darajani, Makoko | 0754490576 | 11 | 35,000 |
| | Matvila Hotel | Mkendo, Mwigobero | 0769659955 | 23 | 25,000 – 200,000 |
| | Setavin Hotel | Mkendo, Mwigobero | 0783335560 | 10 | 50,000 |
| | Grand Victoria Hotel | Kenedy, Iringo | 0681561936 | 20 | 40,000 – 80,000 |
| | Afrilux Hotel | Karume Mwigobero | 0767519476 | 23 | 40,000 |
| | Mlima Mukendo Hotel | Mkendo, Kitaji | 0716922969 | 18 | 30,000 |
| | Orange Tree | Kawawa, Iringo | 0785545833 | 15 | 20,000 – 30,000 |
| | Tembo Beach Hotel | Lakeside, Mkendo | 0713264287 | 7 | 20,000 |
| | Matvila Beach | Lakeside, Mkendo | 0769659955 | 9 | 20,000 – 70,000 |

**B -** Nyumba za kulala wageni Musoma: Daraja la Pili

| NA | JINA LA HOTELI | SEHEMU ILIPO | MAWASILIANO | IDADI YA VYUMBA | GHARAMA YA CHUMBA |
|---|---|---|---|---|---|
| | Parents Motel | Makongoro. Kitaji | 0768883686 | 10 | 15,000 |
| | Kingsport Lodge | Nyakulinga, Mwigobero | 0681561936 | 13 | 16,000 – 35,000 |
| | G&G Hotel | Karume, Mwigobero | 0754000992 | 13 | 15,000 |
| | Bazaar Hotel | Amri Abeid, Kitaji | 0769837772 | 15 | 15,000 |
| | Executive Annex Lodge | Amri Abeid, Kitaji | 0788775401 | 10 | 15,000 |
| | Respect G. House | Mlango mmoja, Nyasho | 0755774690 | 9 | 15,000 |
| | Taratibu G. House | Airport. Nyasho | | 9 | 15,000 |
| | Mujungu Annex | Jamatkhan, Mukendo | 0785629861 | 22 | 15,000 – 20,000 |
| | Donisa Annex | Kenedy, Iringo | 0688363736 | 8 | 15,000 |
| | Recofina G. House | Kenedy, Iringo | 0756758802 | 7 | 15,000 |
| | Up Hill lodge | Mkendo kati Iringo | 0765392626 | 9 | 15,000 |
| | Buhare Ext lodge | Buhare, Buhare | 0754691981 | 6 | 15,000 |
| | Dasaco Inn | Shabani, Kitaji | 0787440383 | 9 | 15,000 – 20, 000 |
| | Stigma Hotel | Mkendo Kati, Iringo | 0754284992 | 15 | 20,000 |
| | Comfort Royal Inn | Mkendo Kati, Iringo | 0784624677 | 10 | 15,000 |
| | Miami Inn | Majita RD, Kamunyonge | 282622203 | 9 | 10,000 – 15,000 |

| NA | JINA LA HOTELI | SEHEMU ILIPO | MAWASILIANO | IDADI YA VYUMBA | GHARAMA YA CHUMBA |
|---|---|---|---|---|---|
| | Munna Lodge | Bondeni, Kamunyonge | | 6 | 15,000 – 20,000 |
| | Diocese of Musoma | Majita RD, Mkendo | | 23 | 8,000 – 18,000 |
| | Diocese of Musoma | CCM RD, Kitaji | | 7 | 8,000 – 18,000 |
| | Magoto Executive Lodge | Shabani Kitaji | 0765033057 | 8 | 15,000 |
| | Kita Executive Lodge | Nyarusurya, Bweri | 0752057836 | 10 | 15,000 |
| | Nine Guest House | Nyarusurya, Bweri | 0787200239 | 9 | 15,000 |
| | Leriam Beach Hotel | Bukanga, Makoko | 0782948764 | 12 | 15,000 – 20,000 |
| | Masai Mara lodge | Rwamlimi, Bweri | 0766560903 | 8 | 15,000 |
| | K&G Guest House | Sanane, Nyakato | 0757321169 | 14 | 15,000 |
| | Ua la Ziwani | Karume, Mwigobero | 07840300289 | 12 | 15,000 |
| | Highway Pack | Bweri, Bweri | | 4 | |
| | Dream Lodge | Songe, Bweri | 0784975077 | 6 | 15,000 |
| | Delta lodge | Iringo, Iringo | | 6 | 7,000 |
| | Maisha lodge | Iringo, Iringo | 0782313961 | 7 | 12,000 |
| | BMT | Bweri, Bweri | | 9 | 10,000 |
| | Masero Inn | Mkendo, Kitaji | 0754398256 | 16 | 10,000 |

**2.** Orodha ya nyumba za kulala wageni Bunda (Umbali kutoka Bunda hadi Butiama ni Kilometa 56 – au usafiri wa takriban nusu saa)

| NA | JINA LA HOTELI | MAWASILIANO | GHARAMA YA CHUMBA |
|---|---|---|---|
| | M. Hotel | 0755 520646 | 30,000 |
| | Part Light Hotel | 0752523270 | 15,000 - 20,000 |
| | Butiama Hotel | 0766326438 | 25,000 |
| | Elephant Hotel | 0756325112 | 15,000 – 30,000 |
| | Heality View Hotel | 0687532090 | 25,000 – 45,000 |
| | Kinamwecho Hotel Road | 0765033057 | 10,000 |
| | Balili Resort | 0766173753 | 80,000- 260,000 |
| | Land Master Hotel | 0765033057 | 35,000 – 50,000 |
| | Kill fat Hotel | 0686629600 | 25,000 – 45,000 |
| | Sill Hotel | 0756839106 | 20,000 |

**3.** Orodha ya nyumba za kulala wageni Butiama

| NA | JINA LA HOTELI | UMBALI KUTOKA (Kutoka Butiama Mjini) katika Kilomita | MAWASILIANO | GHARAMA YA CHUMBA |
|---|---|---|---|---|
| | Mwitongo Lodge | 0.5 | 0782640033 | 30,000 – 50,000 |
| | Isomba Lodge | 13 | | 20,000 |
| | Nyawatu | 1 | | 30,000 |

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Ofisi ya Makamu wa Rais

**Katibu Mkuu**
**Ofisi ya Makamu wa Rais**
**S.L.P 2933**
**Dodoma, Tanzania**
**Simu: + (255) 26 2963149**
**Nukushi: + (255) 26 2963150**
**Barua pepe: ps@vpo.go.tz**